

## Ugiriki ya kale

### Maisha katika majimbo/majiji

Wagiriki walijenga miji yao kwa jumba kubwa/kasri juu ya mlima, na mji wenyewe kwa chini yake. Kuta ndefu za mawe zilijengwa kuzunguka nyumba, karakana/gereji na maduka/masoko, kama sehemu ya ulinzi endapo adui atakapo wavamiwa kukitokea vita. Kila mji ulikuwa na soko la nje/gulio, lililokuwa linaitwa **agora** ambapo watu walikuwa wanakutana na kufanya manunuzi mbalimbali. Ukumbi wa jiji ulikuwepo, na ilikuwa kawaida kwa wanaumme walio huru kwenda na kukutana kuzungumza masuala muhimu. Miji hiyo mara nyingi ilikuwa na uwanja wa michezo na ukumbi wa michezo wa wazi (**friluftsteater**) nje kidogo ya mji. Wagiriki walimaanika kuwa na mwili wenye afya ni muhimu kama ilivyo kwenda kazini na shule.



*På torget i Athen (c Mauricio)*

Nusu ya watu waliokuwa wanaishi katika mji walikuwa ni watumwa. Wengi wao walikuwa wafungwa wa kivita, waliouzwa na kununuliwa kwa pamoja na mahindi, wanyama wa nyumbani na bidhaa nyingine. Wafungwa walifanya kazi za kulima, kwenye migodi na kujenga nyumba. Wafungwa wengine walikuwa ni walimu na waganga/madaktari. Wanawake walioana na wanaume waliokuwa huru. Wanawake walikuwa nyumbani zaidi. Walikuwa na majukumu ya malezi ya watoto na kutoa sadaka kwa miungu.

Watumwa wa kike walipika chakula, kusafisha na kufagia nyumba. Mwanaume ndani ya nyumba alifanya manunuzi yote. Alikuwa anaondoka asubuhi na mapema na harudi tena

mpaka jioni. Akiwa nje anakuwa ananunua vitu anavyohitaji, kuongea/kufanya mazungumzo na wanaume wengine, ama anakwenda kwenye michezo ama kuwinda. Ikiwa alikuwa na wageni nyumbani, mke wake alilazimika kukaa mbali, wakati wageni wakiburudishwa na watumwa wa kike wanaokuwa wakicheza na kuimba.



*En uteskole i Athen (Wiki Commons)*

Wavulana pekee ndio walioruhusiwa kwenda shule. Walianza shule walipokuwa na miaka sita, na kumaliza walipokuwa na miaka kumi na tano (15). Wasichana walibakia nyumbani na kujifunza juu ya kazi za nyumbani na malezi ya watoto. Wasichana wengi waliolewa walipofikia umri wa miaka kumi na tano.

## **Athens**

Wanaume wa Athens walitumia muda mwingi kujadiliana na kuamua jinsi jimbo la jiji linapaswa kuendeshwa na kutawaliwa. Wale walioruhusiwa kusema maoni yao walikuwa ni watu huru na waliokulia kwenye jiji. Kila siku ya tisa (kenda) ilikuwa siku ya mkutano wa watu. Mkutano wa watu ulitengeneza sheria, kuamua kuhusu kodi na kufanya maamuzi muhimu. Maelfu ya watu walijitokeza kushiriki kwenye majadiliano. Sheria moja wapo ilikuwa, mkutano hauwezi kuanza bila ya kuwa na wanachama 6000 (watu watakaojiunga na kushiriki). Wanaume walipiga kura kwa kukubali ama kutokukubali kwa kunyoosha mkono juu. Watu wa Athens waliita ni demokrasia ingawa wanawake, watumwa na wahamiaji hawakuruhusiwa kuamua.



*Den store folketaleren Perikles snakker til borgerne i Athen (Wiki Commons)*

Watu ambao waliongoza mambo/kazi muhimu katika jiji walichaguliwa kwa kutumia mfumo wa kuchagua karatasi ndogo zenye namba/ bahati nasibu. Walitumia mfumo huu wa kuchagua karatasi ndogo zenye namba /bahati nasibu kuchagua mtu atakae toa hukumu/hakimu katika mahakama ama muamuzi wa kwenye michezo. Kila mara moja kwenye mwaka watu wa Athens walipiga kura kuchagua mtu/watu ambao wanataka kuwafukuza/kuwatoa nje ya mji wao. Watu ambao walikuwa hawatakiwi tena kuwepo kwenye mji wa Athen walikuwa kwenye hatari ya kufukuzwa kwenye mji kwa miaka 10.

### **Sparta (wapiganaji)**

Athens mara nyingi ilikuwa vitani dhidi ya Sparta, ambao walikuwa wanachukuliwa kama wapiganaji. Wanaume walikuwa vizuri kupigana kwenye vita, kwa sababu walipata mafunzo ya kuwa wapiganaji. Toka mvulana alipokuwa na miaka saba mpaka miaka 30, waliishi kwenye kambi za kijeshi. Walipata chakula kidogo na nguo mbaya. Njia nzuri ya kuwawezesha kuishi ilikuwa kujifunza kuiba. Spartan waliamini wavulana watakuwa wapiganaji bora kwenye vita kama wakijisikia vibaya. Mtu aliendelea kuwa jeshini mpaka alipofikisha miaka 60 kwa walioweza kufika.



*Gammel statue av spartaner og en moderne utgave (Wiki Commons)*

Wapiganaji toka Sparta walikuwa na nywele ndefu na nguo nyekundu, hivyo ilikuwa rahisi kuwatambua watu hawa maarufu. Ikiwa wapiganaji wao wasingeweza kushinda walitakiwa kupigana mpaka wote wafe. Hawakuruhusiwa kurudi nyumbani kutoka vitani bila ya kushinda.

Wanawake wa sparta walikuwa huru zaidi kuliko wanawake wengine kwenye majimbo ya jiji mengine, kwa sababu wanaume mara nyingi walikuwa wakienda na kukaa mbali na familia zao. Ilikuwa muhimu kwamba wasichana na wanawake wamefundishwa vizuri na wana mwili wenye afya njema ili waweze kuzaa watoto wenye afya. Watoto wakiume walikuwa wakihitajika zaidi, ilikuwa watoto wakike wanatupwa msituni. Mara nyingi walikuwa wanachukuliwa na watu wengine wanakuja kuwafanya kuwa watumwa.

## **Zoezi**

### **Jibu maswali:**

1. Wagiriki walipa itaje sehemu ya soko la nje/gulio ambapo watu wanakutana na kuzungumza kwa pamoja?
2. Nani aliruhusiwa kwenda shule Anthens?
3. Nini kinafanyika katika mkutano wa watu?
4. Jinsi gani walichagua watu wa Athens, watu ambao wangeongoza mambo/kazi muhimu katika jiji lao?
5. Unawezaje kuwatambua wapiganaji kutoka Sparta?